# Wasifu wa Mwanamiti

Ombito Elizabeth Khalili

## Ikisiri

Utungo huu umetungwa kwa heshima ya marehemu Profesa Wangari Maathai, mama mtunza mazingira, aliyejitolea kwa hali na mali kutetea haki, usawa wa jinsi, amani, demokrasia na umoja wa taifa la Kenya. Mama huyo alikuwa mwanamke wa kwanza nchini Kenya kupata shahada ya uzamivu akiwa na umri wa miaka thelathini. Alikuwa mwanamke wa kipekee katika usomi, uhadhiri, utafiti na kamanda mkuu wa jeshi la walinda mazingira. Profesa Wangari, kama tulivyomjua, alikuwa mwanamke wa kwanza barani Afrika kutunukiwa *Tunzo ya Amani ya Nobel* mwaka 2005 kwa kutambua mchango wake adhimu kwa kuzilinda rasilimali za taifa kupitia kuihamasisha jamii mashinani kuishi kwa amani na kuhifadhi mazingira. Kutokana na upendo mkubwa niliokuwa nao kwake, moyo wangu ulifumwa mkuki mkali kwa mauko yake. Ilivyo desturi ya jamii yangu katika maombolezi, nilijikuta nikimlilia huku nikimnuizia maneno mengi. Kilio changu kikageuka kuwa *Wasifu wa Mwanamiti.*

### WASIFU WA MWANAMITI

1. Vyanda vyangu niitikia,
   Kalamu wino nyunyizia,
   Mwanamiti namtungia,
   Liyevuma kikuza miti.

2. Naandika kumsifia,
   Mamangu namkumbukia,
   Uraibu alonachia,
   Fahari kuienga miti.

3. Elufu mosi tisa mia,
   Arobaini shuhudia,
   Njema nyota kumulikia,
   Kazawa mthamini miti.

4. Upesi shule kabishia,
   Na elimu kuipapia,
   Kauli mbiu katungia,
   Maishani kuenzi miti.

5. Dada wengi walififia,
   Usomi walipuuzia,
   Ela mama liazimia,
   Kwa ari kuipanda miti.

6. Sekondari hakukawia,
   Mabuku kuyabukulia,
   Mitihani kajipitia,
   Kamaizi kukuza miti.

7. Ja sumaku alidakia,
   Mafundisho kiyanatia,
   Moyonimwe kadhamiria,
   Raha yake kuona miti.

8. Marekani ulipania,
   Ndege kwayo kuabiria,
   Mzamili kahirimia,
   Purofesa mlea miti.

9. Ujerumani kujafikia,
   Sayansi ikamvutia,
   Mifugo kuwatafitia,
   Ndotoni aliota miti.

10. Shahada kajiangulia,
    Zinalipiku litania,
    Makini akajitungia,
    Falsafa kulinda miti.

11. Lipong’ara mwakademia,
    Zutafindaki ‘kaingia,
    Uhadhiri kasabikia,
    Asahauje hiyo miti?

12. Darasani kifundishia,
    Wakufunzi ’wahudumia,
    Kabambe kuwaandalia,
    Midahalo chini ya miti.

13. Msomea bayolojia,
Wengi kupe kitafitia,
Mara ukajigundulia,
Ubora wa kutunza miti.

14. Chuoni kulipotukia,
Marupurupu kubania,
Wanawake mlitishia,
Kujitetea pamwe miti.

15. Nayo mito liajabia,
Ilivyosomba aridhia,
Malisho yakadidimia,
Kwa kukosa wapanda miti!

16. Mmomonyoko ’lianzia,
Lipokatwa ya asilia,
Wakapanda na kahawia,
Wasisaze wowote mti.

17. Si wasomi mlihofia,
Wana mlo kuutapia,
Filimbi mkatupigia,
Kina dada tupande miti?

18. Kipusa kwao ‘lirudia,
Uzamivu kaangazia,
Mume naye ‘kimchumbia,
Wakiimbiwa nayo miti.

19. Harusini wakaingia,
Wakaijenga familia,
Babangu akamdhania,
Nyondawe taikoma miti!

20. Ulipambwa kihalisia,
Shingoni shanga katungia,
Zilorembwa nyuzi tisia,
Za wavyele walinda miti.

21. Maradufu kazidishia,
Msomi wetu ’lihubiria,
Baragumu kapulizia,
Adinasi wakuze miti.

22. Punde mume ngoa kalia,
Kalemewa ‘mchukulia,
“Mke wangu namkisia,
Kavundikwa mwabudu miti!”

23. “Bure yangu ninajitia,
Siwezani kumkazia!
Uhuru ‘lojitunukia,
Penzi lake lataka miti!”

24. Uzushi kaupalilia,
Matope kumpakulia,
Ukware kamtunukia,
Hamwamini mpenda miti!

25. Virungu alimpigia,
Uhaiwe kautishia,
Hata hewa kampimia,
Bali bui libusu miti.

26. Ndoa kuwa kiungulia,
Virago alijifungia,
Na kwondokea malikia,
Asitazame tena miti.

27. Zilipokithiri kadhia,
Mama talaka litikia,
Lake jina akamwachia,
Heri aitwe Mwanamiti!

28. Kamkanya kumbania,
Kongamano kuhudhuria,
Nguvu tele kazidishia,
Kuhimiza wakuza miti.

29. Japo ndoa kavunjikia,
Jinalo doa ikatia,
Heshima lijisetiria,
Mhadhiri muenza miti.

30. Itikadi lishikilia,
Moyoni kazifumbatia,
Rinda refu ulivalia,
Musitarabu mwanamiti.

31. Usalihina ulobwia,
Misa zote lihudhuria,
Ukabatizwa la Maria,
Imani thabiti ja miti.

32. Maishani litazamia,
Adinasi kuwaminia,
Huku haki kipigania,
Ulimwengu uote miti.

33. Uzohali ulichukia,
Mchapakazi mwenye nia!
Jembe mpini ukatia,
Pasiwe kwekwe kwenye miti.

34. Chama mbasi kaingia,
Kina mama ‘kafurahia,
Kinarani wakamtia,
Awafunze kuhusu miti.

35. Kenya nzima ilisifia,
Mpaka kule Tanzania
Wito ukatajamalia,
Jadhiba ya kukinga miti!

36. Hisani ulizojazia,
Wachochole liwafikia,
Mkanda uliwaundia,
Kawafunga moyoni miti.

37. Chanikiwiti twaringia,
Miche njuga kuivalia,
Na jembe mpini 'metia,
Hamasisha wapanda miti.

38. Vijijini ukapitia,
Wakulima kuwanadia,
Wakaingiwa kwa mamia,
Kikasumba kukuza miti.

39. Laazizi liwatishia,
Wapinzani kakwitikia,
Kwa kuhofu kuangamia,
Sharuti kuilinda miti.

40. Hukuchoka kuwausia,
Kuni wapate kupikia,
Maakuli kuyafurahia,
Wanapoitazama miti.

41. Fito, nguzo wajipatia,
Vitende kuvipigilia,
Na vilango vya kupitia,
Mahabubu mwelewa miti.

42. Manzilini hunakishia,
Na marashi kufukizia,
Si maua yananukia,
Yachanukapo kwenye miti?

43. Watoto wanashabikia,
Mitini kuiparamia,
Matunda wakijitundia,
Vipi wasiisifu miti?

44. Na mizizi watafunia,
Kuzitunza zao afia,
Kivulini wakilalia,
Uhondo umo kwenye miti.

45. Matabibu kiasilia,
Msituni hukimbilia,
Gomba, jani hujikatia,
Muruwa yake dawa miti.

46. Usidhani nakutania,
Loliondo kupasifia,
Mahamumu megugumia,
Wakajaponywa kwayo miti.

47. Miale hatari zuia,
Mahuluki wakumbukia,
Hunayo mbadala njia,
Ila kunawirisha miti.

48. Nchi kavu hutupambia,
Wanyama pori hulishia,
Hata nyuni wakaimbia,
Uhai wetu ndiyo miti.

49. Mamangu hujikumbukia,
Mtoni akikimbilia,
Majini akitumbukia,
Nguo zake juu ya miti.

50. Waziwazi wapasulia,
Wakulima wasosikia,
Udongo kuuhifadhia,
Wakaukinge kwayo miti.

51. Kina nyuki wahadithia,
Mizingani 'limofichia,
Utomvu walambatia,
Maua yarembayo miti.

52. Wangu nina alipania,
Yote miji kuruwazia,
Bustani kujipambia,
Zizidishiwe mingi miti.

53. Makaa usijepalia,
Ukamlaumu Jalia,
Mvua haiji wanyia,
'Kizembea kupanda miti!

54. Kisha mbioni kajitia,
Utawala kuuwania,
Shaukuni wakamtia,
Wasopenda kuona miti.

55. Maji nguo lipovulia,
Kusaka demokirasia,
Ngumu pingu wakakutia,
Kukung'atua kwenye miti.

56. Mbuyu walimkaangia,
Eti hakujisajilia,
Dosari wakamtilia,
Wasitingwe kukata miti.

57. Mapigano likuchachia,
Vichakani ‘lijifichia,
Rozari mkikariria,
Kapita chui kando miti.

58. Naye mama kashikilia,
Penye nia kaona njia,
Bungeni kafululizia,
Wizara ilindayo miti.

59. Kwa ukucha ulipania,
Zikatungwa upya sheria,
Rasilimali kulindia,
Katiba kazingira miti.

60. Hongera mama nakwimbia,
Ahadizo zimetimia,
Wanadamu medhamiria,
Wanaitunza mingi miti.

61. Miche soko kutafutia,
Changamoto ilikuwia,
Mabwanyenye walikawia,
Kuwalipa walea miti.

62. Kuadhimisha ya dunia,
Mazingira ukapangia,
Miche saba kuwapandia,
Mashujaa wa wanamiti.

63. Wangu wa Makeri sikia,
Waiyaki Gori Mahia,
Mekatilili na Mumia,
Mliwakumbuka kwa miti.

64. Visiki walokutupia,
Foresta wakademia,
Usaha wakawatungia,
Wanawake ‘sipande miti.

65. Wanyakuzi ‘liazimia,
Wajenge jumba aushia,
Wachochole kuwabania,
Bustani sibaki mti!

66. Kwa vishindo kawafukia,
Walowezi ‘liwaapia,
Maghorofa kayazuia,
Yasing’oe mikongwe miti.

67. Orofa sitini fikia,
Zingejengwa kifaharia,
Kwa milioni mbili mia,
Dola zing’oe yetu miti!

68. Jumba liwe kwa panda njia,
Serikali kifadhilia,
Wanyonge wakilaania,
Kuyakosa mandhari miti.

69. Jengo refu kupindukia,
Mbili elufu mapakia,
Ya mtemi sanamu pia,
Ipandwe badala ya miti!

70. Wabunge wakakurukia,
Vikumbo wakikupigia,
Wanadada ’kakukimbia,
Was’ambukizwe ndwele miti.

71. Si haya tulotarajia,
Huyu mwehu kutufanyia?
Baba taifa kajutia,
Kamwita kichaa wa miti.

72. Mtukufu katangazia,
Mna mabuu ya mikia,
Vipi ndume mwawawikia,
Vichwamaji waloga miti?

73. Ela mama ulikwamia,
Mashinani kuwafunzia,
Hadi jua likiwachia,
Jasho likilowesha miti.

74. Magazeti liandikia,
Harakati kusawiria,
Wangereza kasailia,
Wakapinga kung’oa miti.

75. Hauchi hauchi kachia,
Kuzighairi mbovu nia,
Bustani likasalia,
Msifurahi wana miti?

76. Nderemo zikashangilia,
Ushindi kuufakamia,
Sondo likawarindimia,
Wasochoshwa kubusu miti.

77. Kaja mama kukulilia,
Wana wao wawe huria,
Ila mkuu wa sheria,
Hakumsikiza mamiti.

78. Vibwebwe mkijifungia,
Vyakula mkivisusia,
Wafungwa mkawalilia,
Jeshi kuu la wanamiti.

79. Hekaluni mkaghuria,
Mishumaa mkiwashia,
Mitutu waliwapigia,
Wasoheshimu wanamiti.

80. Kwa machungu mama walia,
Hata nguo kawavulia
Asikari wariaria,
Laana za walinda miti.

81. Shinikizo lipozidia,
Wafungwa waliwaachia,
Wavyele walikusifia,
Usichoke kupanda miti.

82. Mpenda demokirasia,
Vyama vingi ’lipigania,
Mkahamashisha raia,
Mikononi kibeba miti.

83. Vikaoni kuhudhuria,
Walinzi likufukuzia,
Ja mtawa ukavalia,
Kukwepa wanyongao miti.

84. Penye vita ’lipofikia,
Amani ukahubiria,
Kisasi ukakatazia,
Ukawapa upendo miti.

85. Mahasimu ’liwatakia,
Maridhia kuwafidia,
Korokoroni kakutia,
Waiuwe ari ya miti

86. Vikao wakampangia,
Pembe zake kupunguzia,
Nyuki wakamsukumia,
Katani asipande miti.

87. Matusi walomtupia,
Ya mbwa kasoro mkia,
Mizizi yalinyunyizia,
Yakainawirisha miti.

88. Hila nyongo katumbukia,
Mwilini walimwingilia,
Makuruhu wakamtia,
Kumtenganisha na miti.

89. Kule mbali yakafikia,
Ukwenzi wakausikia,
Kwa mizani wakapimia,
Harakati za mwanamiti.

90. Nalo tuzo kamwangushia,
Amani Nobeli kwa waria,
Dunia kamshangilia,
Muhibu mthamini miti.

91. Oslo ulitahania,
Mboni zikikuangazia,
Halaiki kashuhudia,
Kituzwa kutetea miti.

92. Je usingeling’ang’ania,
Uana kuupigania,
Mwanamke ’ngefikiria,
Kujasitawi pasi miti?

93. Mwanao ninajivunia,
Juhudizo nakuapia,
Mazingira ’lopigania,
Kulinda uhai wa miti.

94. Leo mama ninakwambia,
Chuo kilokufurushia,
Mauko lipoitikia,
Kazindua kozi ya miti!

95. Majonzi yalinivamia,
Saratani kukudandia,
Taksiri ikanitia,
Mauko ukaacha miti.

96. Makiwa menitambalia,
Halili lipojifilia,
Tukakumbwa nayo tanzia,
Kwomboleza mlea miti.

97. Mie hujisikitikia,
Pichayo nikiangalia,
Chozi hunitiririkia,
Niegemeapo kwa miti.

98. Kukubali yako tanzia,
Nzito ja nanga kwa gunia,
Maungoni ninavilia,
Katu sitaikata miti!

99. Kaburini tungekutia,
Na mchanga kukufukia,
Tulitii wako wosia,
Uchomwe tuhifadhi miti!

100. Majivuyo ’mehifadhia,
Takilini kikusalia,
Mola kesha kukumbatia,
Sitahi mbinguni Mamiti.